**REPUBLIC OF RWANDA**

**MINISTRY OF EDUCATION**

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI
## MCHEPUO WA LUGHA (LFK)

Kigali, Agosti 2022

# DIBAJI

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kubwa kutoa Mhutasari huu wa somo la Kiswahili kwa wadau wote. Mhutasari huu ndio waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda. Mhutasari huu umezingatia aina ya mtaala uegemeao katika kujenga uwezo wa mwanafunzi (Mtaala Uegemeao Katika Uwezo). Hivyo, mhutasari huu unatoa mwongozo wa namna ya ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba kunakuwa na aina moja ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika nchi nzima.

Mhutasari huu umezingatia falsafa ya elimu nchini Rwanda ambayo inalenga kuhakikisha kuwa vijana katika kila kiwango cha elimu wanafanikiwa kufikia kilele cha uwezo wao kuhusiana na maarifa sahihi, ujuzi, stadi sahihi na mwenendo mwema wa tabia mwafaka ambao unawajenga na kuwajumuisha katika jamii ili waweze kutumia vilivyo fursa za ajira zilizopo. Ili kuhakikisha kuwepo kwa ubora wa elimu, mhutasari huu umeweka mkazo katika kuhakikisha kuwa mikabala ya mtaala, ufundishaji na ujifunzaji na mikabala ya kiupimaji imefungamanishwa. Hii ni kuhakikisha kwamba mfumo wa elimu unazalisha au kuandaa aina ya raia wanaohitajika au watarajiwao na nchi. Pia, mhutasari huu unazingatia hoja kuwa kuna mambo mengi yanayoathiri kitu ambacho watoto wanafundishwa, ni kwa namna gani wanajifunza ipasavyo na ujuzi waupatao. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na mhutasari sahihi, ubora wa walimu na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo. Hivyo basi, mhutasari huu umeyazingatia vilivyo mambo haya ili kuhakikisha ubora wa elimu. Nia ya kujenga jamii yenye kuegemea katika maarifa na kukua kwa ushindani wa kikanda na kiulimwengu katika soko la ajira, imelazimisha au kuchangia kuhamia katika mtaala uegemeao katika uwezo. Hivyo basi, wanafunzi wakisaidiwa na walimu wao ambao kwa hakika wana wajibu muhimu katika kuhakikisha kuwa muhtasari huu unafanikiwa wanapata stadi na ujuzi sahihi na pia waweze kuyatumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataonesha tofauti siyo tu katika maisha yao bali pia kwa ustawi wa taifa.

Ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote waliochangia katika uandaaji wa waraka huu, hususani REB na wafanyakazi wote walioandaa na kusimamia mchakato wote kuanzia pale ulipoanzia kufika mwisho. Pia, shukrani za dhati ziwaendee wabia wetu wa kimaendeleo waliofadhili zoezi hili kwa kipindi chote.

Tunawaomba wale wote watakaotumia muhtsari huu kutoa maoni yatakayosaidia uboreshaji wake.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote walioshiriki kwa hali na mali katika kutengeneza na kufanikisha muhtasari huu. Muhtasari huu usingeweza kufanikiwa bila kuwepo kwa wadau mbalimbali katika nyanja za elimu walioshiriki kwa hali na mali katika kuugharimia na kuuandika.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee Taasisi na watu walioshiriki kama ifuatavyo:

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi na wafanyakazi wake wote walioshiriki katika uandaaji na uandishi wa muhtasari huu, walimu wote toka chekechea, sekondari hadi Vyuo Vikuu waliochangia katika ufanikishaji wa muhtasari huu.

Shukrani pia zizidi kuwaendea wadau mbalimbali wa Elimu kama: UNICEF, UNFPA pamoja na Aceess to Finance Rwanda kwa kugharimia na kufanikisha shughuli hii.

Tutazidi kushukuru na kuthamini mchango wa mashirika mbalimbali ya Elimu kama CNLG, AEGIS trust, Itorero ry'Igihugu, Gender Monitoring Office, National Unit and Reconciliation Commission, RBS, REMA, Handicap International, Wellspring Foundation, Right To Play, MEDISAR, EDC/L3, EDC/Akazi Kanoze, Save the Children, Faith Based Organisations, WDA, MINECOFIN and Local and International consultants. Msaada wao, ushirikiano wao na ujuzi wao vimekuwa changamoto katika kufanikisha upatikanaji wa muhtasari mpya katika Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR).

**Joan Murungi,**
**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana-REB**

# YALIYOMO

DIBAJI ... i

SHUKRANI ... ii

1. UTANGULIZI ... 1

1.1. Usuli wa mapitio ya mtaala ... 1

1.2. Sababu ya kufundisha na kujifunza Kiswahili nchini Rwanda ... 1

1.2.1. Kiswahili na jamii ... 2

1.2.2. Kiswahili na wanafunzi ... 3

1.2.3. Uwezo ... 3

2. MKABALA WA UFUNDISHAJI ... 6

2.1. Majukumu ya mwalimu ... 6

2.2. Majukumu ya Mwanafunzi ... 7

2.3. Mikakati ya kukabiliana na mahitaji maalumu ya kielimu ... 7

3. MIKABALA YA TATHMINI ... 8

3.1 Aina za tathmini ... 8

3.1.1. Tathmini endelezi ... 8

3.1.2. Tathmini ya jumla ... 9

3.2. Utunzaji wa alama ... 10

3.3. Vigezo katika kuandika tathmini ya jumla ... 10

3.4. Ripoti kwa wazazi ... 11

4. ZANA AU VIFAA VYA UFUNDISHAJI ........ 12
4.1. Orodha ya vifaa au zana zinazohitajika katika ufundishaji ........ 12
4.2. Stadi zinazohitajika kwa mwalimu wa somo la Kiswahili ........ 12
5. MADA ZA UFUNDISHAJI ........ 13
5.1. Muundo wa Mhutasari ........ 13
5.2. Kidato cha nne ........ 14
5.2.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha nne ........ 14
5.2.2. Mada za kidato cha nne ........ 15
5.3. Kidato cha tano ........ 20
5.3.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha tano ........ 20
5.3.2. Mada za kidato cha tano ........ 21
5.4. Kidato cha sita ........ 27
5.4. 1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha sita ........ 27
5.4.2. Mada za kidato cha sita ........ 28
6. MAREJEO ........ 33
7. VIAMBATISHO ........ 34
7.1. Mgawanyo wa vipindi kwa michepuo husika ........ 34

# 1. UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa mapitio ya mtaala

Muhtasari huu wa Kiswahili wa kidato cha 4-6 utatumiwa badala ya ule wa mwaka 2010. Hii ni kutokana na haja ya kuzingatia zaidi mahitaji ya mwanafunzi na kumfanya awe na maarifa, ujuzi na uwezo wa kuyaweka katika vitendo yale aliyojifunza katika mazingira mbalimbali ya kimaisha atakayokumbana nayo. Hii ni tofauti na muhtasari wa awali uliokuwa umeegemea katika madhumuni ya kumfanya mwanafunzi awe na maarifa tu. Hivyo basi, muhtasari huu umeweka msisitizo katika kujenga zaidi stadi na ujuzi kuendana na maudhui yaliyokuwepo katika muhtasari wa awali. Hii ina maana kwamba mtaala huu ni ule uegemeao katika uwezo kama inavyobainishwa katika mpango mkakati wa sekta ya Elimu 2013/14- 2017/2018 (ESSP). Pia, kuna mabadiliko kadhaa ya kimaudhui yaliyofanyika ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kujikita zaidi katika kuwawezesha wanafunzi kuzimudu vema stadi za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika.

Muhtasari huu wa Kiswahili unatoa mwongozo wa maingiliano kati ya mwanafunzi na mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji huku ukibainisha stadi za kivitendo na ujuzi ambao mwanafunzi ataupata wakati anapojifunza na baada ya kufika mwisho wa kila sura au mada ya ujifunzaji.

## 1.2. Sababu ya kufundisha na kujifunza Kiswahili nchini Rwanda

Kiswahili ni lugha ya Afrika inayoozungumzwa na watu wengi barani Afrika na Ulimwenguni kwa ujumla. Jamii ya Rwanda imezungukwa na nchi ambazo zinazungumza Kiswahili. Kwa maana hii, tunahitaji kuwasiliana nao katika nyanja mbalimbali kama kisiasa , kiuchumi na kijamii kwa sababu ni lugha inayootumiwa katika nchi wanachama wa jumuia ya Afrika Mashariki ambapo Rwanda ni mwanachama.

### 1.2.1. Kiswahili na jamii

Lugha ni nyenzo muhimu katika maisha ya binadamu na jamii kwa ujumla kwani humwezesha mtu kufanya mawasiliano kwa madhumuni mbalimbali. Kwa kutumia lugha, binadamu au jamii huwa na fursa ya kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Lugha huweza pia kuunganisha jamii au jamii na jamii nyingine. Kwa namna nyingine, inaweza kubainishwa kuwa lugha ni msingi wa maendeleo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kupitia lugha shughuli mbalimbali za kimaendeleo huchochewa. Lugha pia ni nyenzo muhimu katika kudumisha amani katika jamii yoyote. Hivyo basi, lugha ni wenzo muhimu kabisa unaopaswa kupewa kipaumbele katika jamii yoyote.

Nchini Rwanda kuna lugha nyingine kama vile Kinyarwanda, Kiingereza, na Kifaransa ambazo zinafundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na kwa malengo mbalimbali. Tofauti hizi za malengo au sababu za ufundishaji wa lugha hizi ndio msingi wa kuona umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika kuifundisha na kujifunza nchini Rwanda. Sababu ya msingi ya kufundisha lugha ya Kiswahili ni nafasi ya lugha hiyo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Kiswahili kimepewa nafasi kubwa katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa Rwanda ina ushirikiano na nchi hizi kama vile ushirikiano wa kijamii, kibiashara, na kiutamaduni, lugha ya Kiswahili haiepukiki katika kufanikisha vema ushirikiano huu kuliko lugha nyingine yoyote hususani katika mawasiliano yanayojumuisha jamii pana. Pia inaelezwa kuwa mojawapo ya mashariti ya Rwanda kukubaliwa kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa ni pamoja na kukubali kutumia lugha ya Kiswahili (Kawoya, 2009:7). Mkuthuria, (2006) anaeleza kuwa kifungu cha 19 (d) cha mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kinasisitiza suala la ukuzaji na uendelezaji wa lugha za kiasili hususani lugha ya Kiswahili kama lugha mawasiliano ya ukanda (Lingua Franca). Hii ina maana kwamba wakati Rwanda ilipokusudia kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tayari ilikuwa inajua umuhimu na nafasi ya Kiswahili kama lugha mawasiliano katika ukanda huu. Hivyo basi, mazingira hayo yote yaliyobainishwa ndio msingi mkuu wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.

### 1.2.2. Kiswahili na wanafunzi

Kiswahili ni somo muhimu katika maisha ya wanafunzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba licha ya umuhimu wake katika mawasiliano kwa jumla, Kiswahili kinahitajika katika baadhi ya taaluma au ajira ambazo mwanafunzi anaweza kuingia. Taaluma au ajira hizi ni pamoja na uandishi wa habari, biashara, huduma kwa wateja, uongozaji watalii, ukalimani na tafsiri. Hivyo, somo la Kiswahili linamwezesha mwanafunzi kumudu ipasavyo stadi zote nne za mawasiliano ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa ufasaha katika miktadha tofauti anayoweza kukutana nayo katika maisha yake ya kila siku. Pia, wanafunzi wanapata fursa ya kupata stadi za kushiriki kwa ufasaha katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi. Hii inawasaidia wanafunzi kwa sasa na baadaye katika kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambazo zinahitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kuzifanikisha kwa ukamilifu. Hii ni kwenda sambamba na Progaramu ya Serikali ya Miaka Saba (7YP) 2010 – 2017.

### 1.2.3. Uwezo

Uwezo ni ustadi wa kutekeleza kikamilifu jukumu fulani kwa kutumia maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema. Mtaala huu unampa mwanafunzi fursa ya kuendeleza uwezo wa kimsingi na uwezo wa jumla. Nyaraka za sera za kitaifa, kwa kuzingatia matakwa ya kitaifa, zinabainisha 'Uwezo wa kimsingi pamoja na 'Uwezo wa Jumla' ambao utakuza uwezo wa kufikiri wa hali ya juu.

Uwezo wa msingi umeonyeshwa kama ilivyotajwa katika upana wa uwezo wa somo na kujitokeza katika malengo yaliyoonyeshwa mwaka hadi mwaka kuhusiana na mada zinazofundishwa.

Uchaguzi wa aina za ufundishaji lazima ulenge kuhusu uwezo ambao mwanafunzi ataweza kuuonyesha wakati wowote wa kujifunza hadi atakapohitimu.

Uwezo wa msingi ambao utasisitizwa na kuonyeshwa katika mchakato wa ujifunzaji, umeelezewa kwa ufupi katika aya za chini na

mwalimu atahakikisha kuwa wanafunzi wamepewa majukumu ambayo yatawasaidia kupata stadi hizo.

**Tafakari tunduizi na stadi za utatuzi wa matatizo**: Upatikanaji wa stadi hizi utamsaidia mwanafunzi kufikiri kwa mapana, kutathmini na kutafuta suluhisho kwa matatizo atakayokumbana nayo katika mazingira yoyote.

**Ubunifu na ugunduzi:** Upatikanaji wa stadi hizi utamsaidia mwanafunzi kuamua na kufikiri zaidi ya mawanda ya ufahamu kwa kutoa mawazo mapya na kujenga dhana mpya.

**Utafiti:** Hii itawasaidia wanafunzi kutafuta majibu ya maswali ya msingi kuhusiana na habari na dhana zilizopo na kuelezea hali kuhusiana na utafiti kutoka habari iliyopatikana.

**Mawasiliano katika lugha rasmi:** Walimu watahakikisha matumizi bora ya lugha ya Kiswahili na maelekezo kwa wanafunzi ambayo yatawasaidia kuwasiliana vizuri na kutoa mawazo mwafaka kwa kusema, kuandika na kutumia sarufi sahihi ya lugha na msamiati husika.

**Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha:** Hii itamsaidia mwanafunzi kushirikiana na wenzake katika makundi au katika kazi yoyote atakayopewa, kuwa na mwelekeo chanya na maadili, kuheshimu haki na maoni ya wengine.

**Ujifunzaji wa kudumu**: Upatikanaji wa stadi hizi utawasaidia wanafunzi kupata maarifa na stadi kwa kiwango kinachoweza kuendana na mabadiliko ya maarifa ya kiwango cha juu cha mahitaji binafsi katika maeneo ambayo yanahitaji marekebisho na maendeleo. Kujifunza kiswahili huimarisha na kupanua akili na ni muhimu kwa uendelezaji wa tafakuri tunduizi na hasa tafakari, upimaji na ubinifu. Kwa kusoma vitabu, wanafunzi wataweza kugundua hali za binadamu na kuzama katika uelewa wao kuhusu utamaduni na maadili, masuala ya kijamii katika jamii zao na kutoka tamaduni nyingine ulimwenguni kwani wanafunzi huvutwa na usasa na ukale.

Mada kuhusu maisha yao na dunia waishimo kwa kiwango cha stadi za kufikiri kwa kusoma vitabu na kujifunza lugha itawasaidia kujifunza na kutumia waliyojifunza katika hali halisi.

**Mawanda ya kukuza lugha ya Kiswahili:**

Katika mchakato wa ujifunzaji, mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa:

-Kufanya mawasiliano na watu kutoka katika nchi zinazozungumza Kiswahili,

-Kujieleza kwa kutumia Kiswahili kwa njia ya mazungumzo na kuandika huku akitumia msamiati sahihi na sarufi sahihi inayoendana na kiwango chao cha ujifunzaji na kwa kuzingatia mawasiliano ya kila siku,

-Kusikiliza na kutafsiri taarifa za Kiswahili kwa usahihi,

-Kusoma kwa kujiamini na kuelewa aina mbalimbali za matini za kifasihi na zisizo za kifasihi,

-Kutoa taarifa, mawazo, hisia kwa usahihi na ufasaha katika miktadha mbalimbali ya kijamii na kiutamaduni,

-Kutumia Kiswahili kwa ufasaha anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishajimali nchini Rwanda hususani zile zinazohitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili,

-Kuonesha umilisi mzuri wa msamiati na ruwaza ya lugha ya Kiswahili katika mazungumzo na maandishi,

-Kufanya uhakiki wa kazi yoyote ya kifasihi katika matini andishi au simulizi.

**Kiswahili na ukuzaji wa uwezo**

Nyaraka kuhusu sera ya taifa inayoegemezwa katika matarajio ya taifa inabainisha baadhi ya uwezo wa msingi pamoja na uwezo wa jumla kama inavyobainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Awamu ya Pili (EDPRS 2), Sera ya Sekta ya Elimu (ESP) na katika Mpango Mkakati wa Sekta ya Elimu (ESSP). Ujuzi huu ndio utarajiwao kukuza au kufanikisha ujuzi wa kiwango cha juu cha kufikiri. Pia, ujuzi huu ndio utakaosaidia ujifunzaji wa somo na kuweza kuyatumia yale yaliyofundishwa au kujifunza katika mazingira halisi ya maisha.

Katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili, uwezo wa jumla unapewa kipaumbele sana. Uwezo huu wa jumla ni pamoja na tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti na utatuzi wa matatizo na ushirikiano. Haya yote yanafanikishwa kwa kuhakikisha kuwa mwanafunzi hususani mahitaji yake ndilo linakuwa jambo la msingi katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji washirikiane ili kukamilisha, kufanya tafiti au kutatua changamoto mbalimbali katika maisha kupitia midahalo na majadiliano mbalimbali. Kila ufundishaji na ujifunzaji kwa kila somo lililoandaliwa linazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya maisha. Pia, ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili unatoa nafasi ya kuhakikisha kuwa uwezo wa msingi unajengwa miongoni mwa wanafunzi. Uwezo huu ni kama vile kusoma na kuandika, kuhesabu, mawasiliano katika lugha ya kigeni ambayo ni Kiswahili, sayansi na teknolojia, ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), stadi ya utawala binafsi na mahusiano na watu wengine na zile za maisha, uraia na utambulisho

wa kitaifa, ujasiriamali na uanzishaji wa biashara na ujifunzaji usio na kikomo. Haya yote yanafanikishwa kwa namna ambavyo Kiswahili kinafundishwa na namna wanafunzi wanavyojifunza Kiswahili. Mada mbalimbali zinazojenga muktadha wa kujifunza lugha ni zile zinazokuza ujuzi wa msingi kwa mwanafunzi. Pia, sayansi na teknolojia au ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano inatumika katika kujifunza lugha ya Kiswahili ili kuendana na Mwelekeo wa Rwanda hadi kufikia mwaka 2020 (Vision 2020).

## 2. MKABALA WA UFUNDISHAJI

Kwa kuwa kila mwanafunzi ni wa kipekee na kuwa ana mahitaji yake, kasi ya kujifunza, uzoefu na uwezo, mikakati ya kufundisha lazima iwe mbalimbali lakini yenye mpangilio mzuri wa masomo unaoweza kubadilika ili kuendana na mahitaji ya wanafunzi na aina ya mada inayofundishwa. Pamoja na hayo, mbinu ya kuegemea kwa mwanafunzi katika elimu isichukuliwe kwa maana ya kwamba sasa mwalimu hana wajibu wowote katika kuhakikisha kuwa ujifunzaji unaofanikiwa ipasavyo.

### 2.1. Majukumu ya mwalimu

Mabadiliko ya kuelekea katika mtaala unaoegemea katika uwezo yanahusu mabadiliko ya ujifunzaji, yaani kuhakikisha kuwa ujifunzaji unakuwa wa kina, wa kuvutia na wenye ujenzi wa tabia. Walimu wanajikuta wakihama kutoka katika mbinu ya zamani ya utoaji maarifa na badala yake wanajikuta wakiwa na wajibu wa kuwa wawezeshaji ili kuhakikisha matarijio na mahitaji binafsi ya wanafunzi yanapewa kipaumbele au yanazingatiwa. Kutokana na hali hii, mwalimu anawajibika kubainisha mahitaji ya wanafunzi, namna ujifunzaji utakavyofanyika na namna ya kuongoza tajiriba ya ujifunzaji ipasavyo.

Wajibu wa mwalimu ni kuwaongoza wanafunzi ndani ya darasa na nje ya darasa kushiriki kupitia mbinu mbalimbali shirikishi kupitia mchakato wa ujifunzaji kama mwanafunzi mmoja, katika jozi au katika makundi. Hii inahakikisha kuwa ujifunzaji unakuwa hai na shirikishi, na wenye kuzingatia ushirikiano. Mwalimu atabuni na kuwapatia wanafunzi kazi mbalimbali za kufanya kwa ajili ya majadiliano ya papo kwa papo. Hii ina maana kwamba wajibu wa mwalimu itakuwa ni kutoa mwongozo kwa wanafunzi katika kujenga maarifa yao wenyewe na kuyaweka matendoni.

Wanafunzi wanafundishwa namna ya kutumia vitabu vya ziada na kiada katika namna mbalimbali. Inaweza kuwa kutafiti au kutafuta taarifa na kuzitumia katika kujiandalia notisi zao wenyewe. Hii ni tofauti na mwalimu kuwaandalia wanafunzi notisi.

Mwalimu ni lazima achague kuandaa zana mwafaka za ufundishaji. Zana hizi ni pamoja na mbinu za ufundishaji, chati za kutumiwa na wanafunzi katika kazi zao. Mwalimu ni lazima atoe mfano wa namna ya kusoma au kutamka baadhi ya maneno kabla na wanafunzi wakafuata baadaye. Baada ya mwongozo huo ni muhimu wanafunzi wapewe nafasi ya kutosha katika ujifunzaji. Pia, ni muhimu kwa mwalimu kuandaa mikakati ya kuwawezesha wanafunzi kuendelea kujifunza au kukitumia kile walichojifunza darasani hasa wanapokuwa nje ya darasa. Ni wajibu tena wa mwalimu kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kufanikisha kujifunza somo lililokusudiwa kwa ufanisi.

### 2.2. Majukumu ya Mwanafunzi

Kazi zinazopaswa kufanywa na mwanafunzi zimeoneshwa katika kila mada. Kazi hizi zinaakisi ushirikishwaji mwafaka wa mwanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji. Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji utaongozwa na kusudio la kujenga mazingira rafiki ya mwanafunzi kwa kuzingatia uwezo, mahitaji, uzoefu na mapendeleo. Pia, kazi au shughuli za ujifunzaji zitapangiliwa katika namna ambayo itahamasisha wanafunzi kujenga maarifa akiwa yeye peke yake au katika makundi kwa ushiriki ulio hai. Wanafunzi hufanya kazi zinazowajengea uwezo mahususi katika muundo wa mada zenye zenye malengo mahsusi ya ujifunzaji yaliyogawanyika katika maarifa, stadi na mwenendo mwema. Katika masomo ya vitendo wanafunzi watafanya kazi katika makundi pale ambapo upatikanaji wa vifaa hautaruhusu kufanya kazi peke yao watahimizwa kufanya kazi rahisi kwa kila mwanafunzi peke yake.

### 2.3. Mikakati ya kukabiliana na mahitaji maalumu ya kielimu

Kila Mnyarwanda anayo haki ya kupata elimu bila kujali tofauti za mahitaji zilizopo. Msingi wa yote haya ni kuonyesha kuwa raia wote wanafaidika kutokana na mpago wa elimu uliopo. Uwezekano wa fikra hii ni kulenga hasa katika mahitaji ya elimu. Ugumu wa

haya ni kwamba tunao raia/wanafunzi ambao wanatofautiana katika hali zao kimaisha na wengi wasiopendelea elimu. Tofauti zinaweza kuwa hisia, mabavu, nyanja za fahamu zinazolenga katika mgongano wa elimu ya ukale zinazojulikana kama utahira.

Wanafunzi wote hawa wana haki sawa ya kufaidi kutokana na mfumo wa msingi wa lazima wa elimu wa kila siku katika sehemu zao. Kwa maana hii, majukumu ya shule ni kuwaorodhesha na kupanga mikakati ya kumpa kila mtu elimu inayomfaa katika mchakato wa kusoma na kujifunza. Mikakati na masharti ya tathmini inapaswa pia kusawazishwa kulingana na mahitaji ya wanafunzi hawa. Mwongozo wa kina kwa kila kategoria ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu yametolewa katika mwongozo kwa walimu.

## 3. MIKABALA YA TATHMINI

Tathmini ni mchakato wa kupima ufundishaji na ujifunzaji kwa kukusanya na kutafsiri vigezo binafsi vya maendeleo ya mwanafunzi binafsi katika mchakato wa kujifunza na kufanya uamuzi kuhusu mafanikio ya mwanafunzi yanayopimwa dhidi ya viwango vilivyoainishwa. Tathmini ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika mtaala mpya unaoegemea katika uwezo, tathmini inapaswa izingatie uwezo ambapo mwanafunzi atapewa mazingira tofauti au magumu yanayohusiana na maisha yake ya kila siku na kuombwa atumie aliyojifunza katika kupambana au kujitatulia matatizo aliyokumbana nayo.

Tathmini itapangwa au kufanywa katika ngazi zifuatazo: Tathmini katika ngazi za shule; mitihani ya wilaya; tathmni ya kitaifa (LARS) na mtihani wa taifa.

### 3.1 Aina za tathmini

### 3.1.1. Tathmini endelezi

Tathmini endelezi inatumia mbinu rasmi na zisizo rasmi zitumikazo shuleni kuangalia kama ujifunzaji unafanyika kama inavyokusudiwa au la. Wakati mwalimu anapoandaa somo lake anapaswa kuonyesha vigezo vya ufaulu na mabadiliko ya mwenendo anapoanza kufundisha sura mpya. Baada ya kumaliza kila mada ,mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamemudu

yaliyoongelewa katika ujuzi upatikanao katika kila mada kabla ya kuanza kujifunza mada inayofuata. Mwalimu atapima jinsi kila mwanafunzi atakavyomudu vizuri somo lake pamoja na tafakuri tunduizi zilizoelezwa katika muhtasari. Kutokana na haya mwalimu atapata picha halisi kuhusu maendeleo ya ujifunzaji wa wanafunzi. Mwalimu atatumia moja au mchakato wa yafuatayo (a) Utafiti (b) Kalamu na Karatasi (c) Maswali dodoso au majaribio ya kuzungumza.

### 3.1.2. Tathmini ya jumla

Tathmini ya jumla hutoa picha ya uwezo au mwelekeo maalum kwa muda fulani wa ufundishaji na ujifunzaji. Makusudi muhimu ya tathmini ya jumla ni kutathmini kuwa malengo ya kujifunza yamefikiwa. Tathmini ya muhtasari inatoa picha ya umahiri au maendeleo ya mwanafunzi wakati wowote maalum na kutumia matokeo hayo kwa kurekodi au kutoa uamuzi wa maendeleo yake ili aweze kuchaguliwa katika ngazi nyingine ya elimu au apewe cheti. Tathmini hii ni lazima iweke pamoja mwelekeo au maoni ambapo mwanafunzi ataweza kuonyesha alivyomudu uwezo wote alioupata katika ujifunzaji.

Inaweza ikawa upimaji shuleni au nje ya shule kwa muundo wa mitihani wa taifa. Upimaji wa jumla shuleni hususani ule wa kila mtihani wa somo unapaswa kufanyika mara moja mwishoni mwa kila muhula wa masomo na mara moja tena mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Wastani wa matokeo ya upimaji wa jumla shuleni kwa kila somo utapimwa, kurekodiwa na kuwekwa miongoni mwa matokeo ya mtihani wa mwisho wa kitaifa .

Wastani wa upimaji wa jumla shuleni utachangia asilimia fulani pindi walimu watakapopata uzoefu na kujiamini katika nyanja za upimaji na itakapofikia mwaka wa tatu katika utumiaji au uendelezaji wa mtaala mpya, wastani utachangia asilimia kumi (10%) katika mtihani wa mwisho, hii itaenda hatua kwa hatua . Wilaya zitahamasishwa au kuungwa mkono kuendeleza ubunifu na kupanga mitihani ya kawaida kwa madarasa kwenye shule zote kwa kutathmnini matokeo na mafanikio ya wanafunzi katika kila shule. Upimaji nje ya darasa utafanyika mwishoni mwa kidato cha tatu na cha sita.

### 3.2. Utunzaji wa alama

Huu ni ukusanyaji wa vigezo vya ukweli na thabiti kutoka vyombo vya upimaji na kuvitumia katika uchunguzi kuhusu ufaulu wa mwanafunzi kwa kuonyesha vigezo vilivyowekwa. Vigezo vyovyote vya tathmini vitakavyotumiwa vitatoa data katika muundo wa matokeo ambao utarekodiwa na kuhifadhiwa vizuri katika faili kwa sababu zitachangia katika maendeleo ya mwanafunzi na itakuwa kumbukumbu kwa mwanafunzi pamoja na wazazi kwa kuangalia maendeleo ya ujifunzaji wake na kumpa ushauri kulingana na mtihani wa mwisho wa wanafunzi .

Faili hili linahifadhi kazi zilizofanywa na mwanafunzi katika tathmini mbalimbali na kuonesha pale ambapo amefaulu vizuri au alipokuwa na udhaifu. Faili hili halionyeshi tu kazi zilizofanyika (kama karatasi na majaribio) bali linaonyesha pia rekodi za mazoezi yaliyofanyika kwa muda mrefu kama sehemu ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Faili hili litatumika kuchunguza ikiwa matokeo ya mwanafunzi kuhusu kazi au tathmini mbalimbali alizofanya darasani yanatosha kabla ya kufanya tathmini ya jumla kwa kila somo.

### 3.3. Vigezo katika kuandika tathmini ya jumla

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, mpango wa kile kitakachoulizwa lazima uandaliwe kwa kuonyesha mada husika, idadi ya maswali kwa kila kiwango cha “Taksonomia ya Bloom” na kuonyesha alama zilizopangwa kwa kila swali. Katika mtaala uegemeo katika uwezo, maswali ya kiwango cha juu cha “taksonomia ya Bloom” yanapewa uzito kuliko yale ya kiwango cha chini (maarifa na ufahamu).

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, mtahini lazima ahakikishe kuwa jaribio au maswali ya mtihani yamepangwa sambamba na upimaji wa uwezo wa mwanafunzi kwa kufanya yafuatayo:

-Kutambua mada za kuuliza kutoka muhtsari kulingana na somo,

-Kufupisha yaliyomo katika somo ukifikiria kuwa ndio msingi wa zoezi,

-Kutambua matokeo ya ujifunzaji yatakayopimwa katika zoezi,

-Kuandaa jedwali la mambo muhimu yanayotakiwa.

-Kuhakikisha kuwa vitenzi vilivyotumiwa katika uandaaji wa maswali havihitaji kumbukumbu kukumbuka pekee yake bali vinapima mawanda ya uwezo kama ilivyoonyeshwa katika muhtasari.

**Muundo wa mtihani wa Kiswahili kidato cha 4-6 mchepuo wa lugha**

Baada ya mwisho wa masomo kutakuwepo mitihani miwili kama ifuatavyo :

**Mtihani wa kwanza (1)**

Mtihani wa kwanza utakuwa nasehemu zifuatazo: Sehemu ya kwanza:Ufahamu , Sarufi ,Utungaji

**Mtihani wa pili (2)**

Mtihani wa pili utakuwa na sehemu zifuatazo:

Sehemu ya A: Nadharia ya Fasihi

Sehemu B: Uhakiki wa tanzu za fasihi katika Kiswahili

**3.4. Ripoti kwa wazazi**

Ufundishaji na ujifunzaji unaoegemea katika uwezo unapaswa kushirikisha wazazi ili waelezwe kuhusu hali ya ujifunzaji wa watoto wao. Ripoti ya shule iliyo muhimu zaidi ni ile inayoshirikisha wazazi ili kuoneshwa wazi pale wanafunzi hufanya vizuri na pale ambapo wanahitaji kuboresha.

Mbali na ripoti ya shule, faili la mwanafunzi lazima lionyeshe matokeo, tabia, mwenendo, na sifa zake kutoka kwa walimu ili wazazi watoe mrejesho kwa uongozi wa shule.

## 4. ZANA AU VIFAA VYA UFUNDISHAJI

### 4.1. Orodha ya vifaa au zana zinazohitajika katika ufundishaji

Sehemu hii inajadili vifaa vinavyohitajika ili utekelezaji wa muhtasari huu uweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Katika ufundishaji huu wa somo la Kiswahili kunahitajika vifaa au zana mbalimbali ili kukabiliana na mahitaji maalumu katika elimu. Baadhi ya vifaa ambavyo vinaweza kutumika mara kwa mara ni pamoja na redio, picha za vifaa na vitu mbalimbali katika mazingira mbalimbali, picha za watu wa marika mbalimbali wakiwa katika miktadha tofauti, simu ya mkononi, kanda za sauti zenye mazungumzo na hotuba za Kiswahili, vitabu, matini au vifungu mbalimbali vya mazungumzo.

### 4.2. Stadi zinazohitajika kwa mwalimu wa somo la Kiswahili

Mwalimu wa Kiswahili anapaswa kuwa na stadi, maadili na sifa zifuatazo:

-Kushirikisha wanafunzi katika kazi mbalimbali za ujifunzanji,

- Kutumia mbinu na mikabala mbalimbali ya ufundishaji na tathmini,

- Kutumia maelekezo yanayolingana na kiwango cha ujuzi wa wanafunzi,

- Kuwa na ubunifu na ugunduzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji,

- Kuhusianisha somo lake na masomo mengine,

- Kuwa na uwezo wa kuratibu na kuwasiliana vizuri na wanafunzi, walimu wenzake, wazazi na uongozi wa shule kwa ujumla,

- Kuwa kiongozi na mshauri,

- Kuonyesha shauku na upendo usio na upendeleo kwa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji,

- Kuwa na uwezo wa kufundisha mada zilizoandaliwa katika muhtasari huu wa Kiswahili,

-Kuwa na mwelekeo mzuri wa nidhamu.

## 5. MADA ZA UFUNDISHAJI

### 5.1. Muundo wa Mhutasari

Muhtasari huu una sehemu kuu nane ambazo ni utangulizi, malengo ya jumla mwishoni mwa kila kiwango, mikabala ya mbinu za ufundishaji, mikabala ya upimaji, vifaa vya ufundishaji, mada za muhtasari, marejeleo na viambatanisho. Sehemu hizi ni utangulizi na mada za muhtasari. Vipengele vinavyojitokeza katika utangulizi ni pamoja na usuli, sababu za ufundishaji Kiswahili nchini Rwanda, uwezo wa jumla na mwenendo mwema utarajiwao kwa wanafunzi. Kila mada ya muhtasari imeundwa na jedwali. Jedwali hili lina safu tano zinazohusika na ufundishaji na ujifunzaji wa mada inayobainishwa katika jedwali husika. Safu ya kwanza inahusika na maarifa na ufahamu. Kiwango hiki kinahusu ushughulishaji wa akili ya mwanafunzi katika kiwango cha chini cha kazi kama kurudia, kueleza, kutaja, kuonesha, n.k. Hiki ni kiwango cha chini cha fikra kwa mujibu wa ufafanuzi wa Bloom. Safu ya pili inahusika na kiwango cha juu sana cha fikra kwa mujibu wa ufafanuzi wa Bloom. Kiwango hiki kinahusu ushughulishaji wa akili ya mwanafunzi katika kiwango cha juu cha kazi kama uchambuzi, ufafanuzi, kufanya muhtasari, kutathmini, kutumia mifano, n.k. Safu ya tatu inahusika na maadili na mwenendo mwema unaokusudiwa kujengwa kwa mwanafunzi kupitia mada inayofundishwa. Safu ya nne inahusu yaliyomo. Haya ni maudhui ya msingi yanayokusudiwa kufundishwa katika mada husika ili kufikia malengo ya kimaarifa na ufahamu, stadi na hata mwenendo mwema. Safu ya tano inahusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hizi zimeegemezwa katika kazi atakazozifanya mwanafunzi ili kukamilisha mchakato wa ujifunzaji.

Jedwali hili pia lina safu mlalo zilizopangwa ifuatavyo: Uhusiano wa mada husika na mada nyingine katika masomo mengineyo, vigezo vya tathmini au upimaji, na zana au vifaa vya ufundishaji wa mada husika.

Muhtasari huu wa kidato cha nne hadi cha sita una jumla ya mada 13; kidato cha nne kina jumla ya mada tano, kidato cha tano mada nne na kidato cha sita mada nne.

| | **Kidato cha 4** | **Kidato cha 5** | **Kidato cha 6** |
|---|---|---|---|
| Mada kuu | 5 | 4 | 3 |
| Mada ndogo | 5 | 4 | 4 |

## 5.2. Kidato cha nne

### 5.2.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha nne

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha nne ataweza:

-Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali,

-Kuandika aina mbalimbali za insha za kimasimulizi,

-Kuelewa na kuelezea dhima ya lugha katika jamii,

-Kueleza asili, kukua, na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki,

-Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi hususani utanzu wa hadithi,

-Kuainisha na kubainisha tanzu za fasihi ya Kiswahili na kueleza dhima ya fasihi katika jamii,

-Kusoma na kuelewa maandiko na vitabu mbalimbali vya Kiswahili vyenye taarifa ndefu ili kupata ujumbe uliomo,

-Kusikiliza na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii,

-Kubaini matumizi sahihi ya maneno katika tungo mbalimbali za Kiswahili.

### 5.2.2. Mada za kidato cha nne

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA KUU** | | | | **MADA NDOGO** |
| **LUGHA NA JAMII** | | **LUGHA YA KISWAHILI** | | **IDADI YA VIPINDI: 28** |
| **Uwezo mahsusi wa mada**: Kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa umuhimu wa lugha kama chombo cha mawasiliano katika jamii, kuenea kwake na kutumia kwa usahihi hali ya masharti -nge- | | | | |
| **Malengo ya ujifunzaji** | | | | |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | **Yaliyomo** | **Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji** |
| ➢ Kufafanua maana ya lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano.<br>➢ Kutaja maeneo ya asili ya lugha ya Kiswahili na chimbuko lake barani Afrika.<br>➢ Kuelezea njia ya Kiswahili katika kuenea kwake<br>➢ Kubainisha viambishi vya hali ya masharti - nge - | • Kueleza kimazungumzo na kimaandishi maana ya lugha na kutetea umuhimu wake katika jamii.<br>• Kueleza asili ya lugha ya Kiswahili, chimbuko lake pamoja na athari zake katika lugha nyingine.<br>• Kuonesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili toka pwani hadi Rwanda.<br>• Kutunga sentensi tofauti au kusimulia juu ya kisa fulani kwa kutumia hali ya masharti -nge-. | ○ Kujivunia umuhimu wa lugha katika jamii.<br>○ Kuimarisha desturi ya raia wa bara la Afrika, hususan raia wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutumia lugha ya Kiswahili.<br>○ Kujenga ushirikiano kati ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.<br>○ Kufurahia matumizi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia kanuni za kisarufi. | ▪ Maana ya lugha na umuhimu wake<br>▪ Asili ya lugha ya Kiswahili na chimbuko lake<br>▪ Kuenea kwa lugha ya Kiswahili<br>▪ Sarufi: Matumizi ya viambishi vyenye dhana ya masharti -nge- | - Katika jozi, wanafunzi wazungumzie: (a) maana ya lugha na umuhimu wake; (b) umuhimu wa Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.<br>- Katika makundi, wanafunzi wajadili kuhusu asili ya Kiswahili na chimbuko lake<br>- Katika makundi, wanafunzi wafanye utafiti kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili toka Pwani hadi Rwanda.<br>- Katika jozi, wanafunzi watetee faida na hasara za kutumia lugha moja ndani ya nchi.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia hali ya masharti - nge- |
| ***Uhusiano wa mada na masomo mengine:*** *Masomo ya historia, isimu, sosiolojia na mengineyo yanayohusika na mila na desturi za jamii* | | | | |
| ***Zana/Vifaa:*** *Vitabu kuhusu historia ya Kiswahili, mitandao ya intaneti, majarida, ramani ya Afrika yenye ukanda wa Mashariki, Bahari ya Hindi na visiwa vilivyoko kwenye ukanda huu.* | | | | |
| ***Zana/Vifaa:*** *Vitabu kuhusu historia ya Kiswahili, mitandao ya intaneti, majarida, ramani ya Afrika yenye ukanda wa Mashariki, Bahari ya Hindi na visiwa vilivyoko kwenye ukanda huu.* | | | | |

<table>
<tr><th colspan="2">MADA KUU</th><th colspan="3">MADA NDOGO</th></tr>
<tr><th colspan="2">LUGHA KATIKA SANAA</th><th colspan="2">FASIHI KATIKA KISWAHILI</th><th>IDADI YA VIPINDI: 44</th></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kueleza fasihi katika Kiswahili kwa ujumla kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano ndani yake; Kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya LI-YA.</td></tr>
<tr><th colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</th><th rowspan="2">Yaliyomo</th><th rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</th></tr>
<tr><th>Maarifa na ufahamu</th><th>Stadi</th><th>Maadili na mwenendo mwema</th></tr>
<tr><td>➢ Kufafanua maana ya sanaa na dhima yake katika jamii.<br><br>➢ Kuelezea dhana ya fasihi na dhima yake katika jamii.<br><br>➢ Kubainisha tanzu za fasihi simulizi na kuonesha mchango wa kila tanzu katika maendeleo ya nchi.<br><br>➢ Kubainisha majina ya ngeli ya LI – YA -</td><td>• Kueleza kimazungumzo na kimaandishi maana ya sanaa na kutetea umuhimu wake katika jamii.<br><br>• Kutetea dhima ya fasihi katika mafanikio ya jamii.<br><br>• Kueleza dhana ya fasihi simulizi na kutofautisha tanzu zake.<br><br>• Kutumia kwa usahihi viambishi nafsi vya majina ya ngeli ya LI – YA – katika umoja na wingi.</td><td>○ Kuiheshimu sanaa katika ujenzi wa jamii na maendeleo yake.<br><br>○ Kuimarisha fasihi kama kazi ya sanaa inayorahisisha mawasiliano katika jamii.<br><br>○ Kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kama maktaba ya utamaduni wa jamii.<br><br>○ Kujivunia matumizi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia kanuni za kisarufi.</td><td>▪ Sanaa na dhima yake katika jamii.<br><br>▪ Dhana ya fasihi na umuhimu wake katika jamii<br><br>▪ Dhana ya fasihi simulizi na tanzu zake<br><br>▪ Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA -</td><td>- Katika jozi, wanafunzi wazungumzie: (a) maana ya Sanaa; (b) umuhimu wa sanaa katika jamii.<br><br>- Katika makundi, wanafunzi wajadili: (a) maana ya fasihi; (b) umuhimu wa fasihi katika maendeleo ya jamii ya Wanyarwanda katika muktadha wa amani, umoja na maridhiano, uzalendo, usawa wa jinsia, n.k.<br><br>- Katika makundi, wanafunzi washughulikie: (a) dhima ya fasihi simulizi; (b) lengo la fasihi simulizi; (c) mchango wa tanzu za fasihi simulizi katika elimu kwa Wanyarwanda;<br>(d) madhara ya fasihi inavyotumiwa vibaya, mfano wa Rwanda kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi achague tanzu moja ya fasihi simulizi anayoipenda na atetee maoni yake.<br><br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge kifungu cha habari kifupi kwa kutumia majina ya ngeli ya LI-YA- aliyopewa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la Fasihi katika Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda; Somo la Isimu jamii.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kueleza kwa urahisi kimazungumzo na kimaandishi umuhimu wa fasihi; vipenegele vyake na mchango wa vipengele hivi katika maendeleo ya jamii; Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya LI-YA- katika umoja na wingi kwa kuzingatia kanuni za kisarufi husika.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Vitabu kuhusu fasihi ya Kiswahili, Makala kuhusu tanzu za fasihi simulizi, mitandaoo ya intaneti, taarifa zilizorekodiwa, vinasasauti, tarakilishi.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td colspan="3">MADA KUU</td><td colspan="2">MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="3">UHAKIKI WA HADITHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI</td><td>MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI</td><td>IDADI YA VIPINDI: 60</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kutoa muhtasari wa hadithi na kuchambua kifani na kimaudhui hadithi za Kiswahili; kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya PA-M-KU-</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</td><td rowspan="2">Yaliyomo</td><td rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</td></tr>
<tr><td>Maarifa na ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td></tr>
<tr>
<td>➢ Kubainisha sifa na taratibu za kutoa muhtasari mzuri.<br>➢ Kueleza dhana ya fani katika fasihi simulizi.<br>➢ Kueleza dhana ya maudhui katika hadithi simulizi.<br>➢ Kubainisha vipera muhimu katika uchambuzi wa hadithi simulizi.<br>➢ Kutambua majina ya ngeli ya PA-M-KU</td>
<td>• Kueleza kimazungumzo na kimaandishi dhana ya muhtasari, sifa zake na taratibu za kutoa muhtasari mzuri.<br>• Kufafanua dhana ya fani katika hadithi simulizi.<br>• Kujadili dhana ya maudhui katika hadithi simulizi.<br>• Kuchambua hadithi simulizi kwa kuzingatia vipera muhimu vya uchambuzi.<br>• Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina ya ngeli ya PA-M-KU</td>
<td>○ Kujenga tabia ya uwazi, usahihi na kuzungumza au kuandika kwa ufupi.<br>○ Kukuza tabia ya kusoma makala mbalimbali na kuchambua fani yake.<br>○ Kujenga uzoefu wa kuchambua kazi za fasihi kwa ajili ya maudhui.<br>○ Kuendeleza akili, tafakuri tunduizi, stadi za tathmini katika maisha ya kila siku.<br>○ Kujivunia matumizi ya Kiswahili sanifu katika mawasiliano ya kila siku.</td>
<td>▪ Dhana ya muhtasari, sifa zake na taratibu za kutoa muhtasari mzuri<br>▪ Dhana ya fani katika hadithi simulizi<br>▪ Dhana ya maudhui katika hadithi simulizi.<br>▪ Uhakiki wa hadithi simulizi<br>▪ Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU pamoja na vivumishi ambatana.</td>
<td>- Katika jozi, wanafunzi wazungumzie: (a) dhana ya muhtasari; (b) taratibu za kutoa muhtasari mzuri.<br>- Katika makundi, wanafunzi wajadili: (a) maana ya fani;<br>(b) vipengele vya fani; (c) faida ya kutoka uchambuzi wa fani.<br>- Katika makundi, wanafunzi wajadili: (a) maana ya maudhui; (b) vipengele vya maudhui;<br>(c) nafasi ya maudhui katika kazi ya fasihi.<br>- Katika makundi, wanafunzi wachambue hadithi walizopewa (zinazohusiana na uzalendo, ushirikiano, maridhiano, uwajibikaji, n.k.),watoe muhtasari, fani na maudhui.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi:<br>(a) atunge hadithi fulani na kuifanyia uchambuzi;<br>(b) achague yeye mwenyewe hadithi fulani na kuisimulia hadharani.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge kifungu cha habari kifupi kwa kutumia majina ya ngeli ya PA-M-KU</td>
</tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo kuhusu uchambuzi wa vifungu vya habari katika Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda; Somo la Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kuchambua kwa ukamilifu hadithi simulizi kwa kuzingatia muhtasari, fani na maudhui; Kutunga na kusimulia hadithi simulizi; Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya PA-M-KU- katika umoja na wingi kwa kuzingatia kanuni za kisarufi husika.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Vitabu kuhusu uchambuzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili, Makala kuhusu tanzu za fasihi simulizi, mitandaoo ya intaneti, vinasasauti, tarakilishi.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td colspan="2">MADA KUU</td><td colspan="3">MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="2">UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO</td><td colspan="2">MDAHALO NA MJADALA</td><td>IDADI YA VIPINDI: 44</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kuzungumza kwa ufasaha kwenye midahalo na mijadala kwa kuzingatia mada zilizotolewa; Kutumia kwa usahihi hali ya kuamrisha/kushurutisha.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</td><td rowspan="2">Yaliyomo</td><td rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</td></tr>
<tr><td>Maarifa na ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td></tr>
<tr><td>➢ Kueleza dhana ya mdahalo na mjadala pamoja na lengo lake.<br>➢ Kubainisha taratibu za kuandaa mdahalo<br>➢ Kutambua mbinu za kuandaa mjadala.<br>➢ Kutambua viambishi vya vitenzi vinavyoleta dhana ya kutoa amri au hali ya kushurutisha.</td><td>• Kueleza kimazungumzo na kimaandishi dhana ya mdahalo na mjadala.<br>• Kuandaa mdahalo kwa kuzingatia taratibu muhimu.<br>• Kuandaa mjadala kwa kuongozwa na mbinu husika.<br>• Kutoa amri kwa watu mbalimbali.</td><td>○ Kuimarisha tabia ya kutumia kamusi kwa kuchunguza maana za msamiati.<br>○ Kuonesha moyo wa heshima, ushirikiano na uajibikaji wakati wa mdahalo.<br>○ Kuonesha adabu, utulivu, akili na hali ya kujiamini wakati wa mjadala.<br>○ Kuonyesha nia ya kutumia hali ya kuamrisha/kushurutisha kwa usahihi katika mazungumzo.</td><td>▪ Nadharia ya mdahalo na mjadala.<br>▪ Uandaaji wa mdahalo<br>▪ Uandaaji wa mjadala<br>▪ Sarufi: Hali ya kuamrisha/kushurutisha kwa vitenzi umoja na wingi.</td><td>- Katika jozi, wanafunzi wachunguze kutoka Kamusi Sanifu ya Kiswahili au mitandao ya intaneti nadharia ya mdahalo na mjadala.<br>- Katika makundi, wanafunzi:<br>(a) wasikilize au wasome mdahalo uliorekodiwa;<br>(b) washiriki kwenye mdahalo kulingana na mada walizopewa na mwalimu.<br>- Katika makundi, wanafunzi washirikishwe kwenye mjadala kuhusu mada zifuatazo: (a) mchango wa wazazi katika malezi ya watoto wao; (b) sera ya kisiasa ya “malezi kwa wote”; c) masuala yanayoiangamiza jamii kama vile matumizi ya dawa za kulevya, Ukimwi, n.k.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge kifungu cha habari kifupi kwa kutumia vitenzi alivyopewa katika hali ya kushurutisha/kuamrisha.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la midahalo, mijadala katika Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kushiriki kwa ukamilifu kwenye midahalo na mijadala na kuzungumza kwa ufasaha wakati wa kutoa hoja kwa kuzingatia maagizo husika; Kutumia kwa usahihi hali ya kuamrisha.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Redio rekoda, vinasasauti, tarakilishi, flash disk, midahalo na mijadala iliyorekodiwa, projekta.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td colspan="3">MADA KUU</td><td colspan="2">MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="3">UTUNGAJI</td><td>INSHA ZA MASIMULIZI AU KUBUNI NA UANDISHI WA RIPOTI</td><td>IDADI YA VIPINDI: 40</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari kimazungumzo; Kuandika ripoti na kuiwasilisha hadharani; Kutumia kwa usahihi usemi asili na usemi wa taarifa.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</td><td rowspan="2">Yaliyomo</td><td rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</td></tr>
<tr><td>Maarifa na ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td></tr>
<tr><td>➢ Kutoa maana ya insha na kubainisha aina zake.<br>➢ Kueleza insha za masimulizi pamoja na mwongozo wa uandaaji wake.<br>➢ Kuelezea ripoti pamoja na mbinu za utungaji wake.<br>➢ Kubainisha sehemu muhimu katika uandishi wa ripoti.<br>➢ Kutambua mabadiliko yaliyoko kati ya usemi wa asili na usemi wa taarifa.</td><td>• Kueleza kimazungumzo na kimaandishi dhana ya insha katika Kiswahili.<br>• Kuandaa insha ya masimulizi kwa kuzingatia taratibu muhimu za utungaji.<br>• Kujadili kimazungumzo na kimaandishi nadharia ya ripoti katika Kiswahili<br>• Kuandika ripoti katika Kiswahili kulingana na mbinu maalum za utungaji.<br>• Kumnukuu mtu kwa kuzingatia kanuni za usemi husika.</td><td>○ Kuimarisha tabia ya kusoma maandishi tofauti ili kukuza ujuzi na uwezo.<br>○ Kukuza tabia ya kufurahia kazi za ubunifu katika kujadili mambo na kutatua matatizo mbalimbali.<br>○ Kuridhika na mitindo ya lugha tofauti katika kazi za utungaji.<br>○ Kuendeleza akili au kipaji cha mtiririko wa fikra katika ubunifu wa maandishi mbalimbali.<br>○ Kuboresha tabia ya kusanifisha lugha kimaandishi.</td><td>▪ Nadharia ya insha katika Kiswahili<br>▪ Insha za masimulizi na uandaaji wake<br>▪ Nadharia ya ripoti<br>▪ Uandishi wa ripoti<br>▪ Sarufi: Usemi asili na usemi wa taarifa</td><td>- Katika jozi, wanafunzi wazungumzie nadharia ya insha na mifano mbalimbali ya insha zinazojulikana kwao.<br>- Katika makundi, wanafunzi wasome insha tofauti kutoka vitabuni na kuzitolea mhadhara darasani;<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge insha ya masimulizi kuhusu mada mbalimbali kama vile safari, ugonjwa wa Ukimwi, kazi za umuganda, usafi, madawa ya kulevya, uvivu, n.k.<br>- Katika jozi, wanafunzi wajadiliane kuhusu ripoti, sehemu kuu zake pamoja na lengo lake.<br>- Katika makundi, wanafunzi: (a) wafikirie mkutano mmoja waliowahi kuhudhuria au kusikia na kuutolea ripoti;<br>(b) wasahihishe ripoti yenye makosa ya kimuundo.<br>- Katika jozi, wanafunzi wabadilishe sentensi zenye usemi wa asili katika usemi wa taarifa na kinyume chake.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la mdahalo, mjadala katika Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari kwa njia ya mazungumzo; Kuandika ripoti na kuiwasilisha hadharani; Kutumia kwa usahihi usemi asili na usemi wa taarifa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Vitabu kuhusu insha, Kamusi ya Kiswahili sanifu, tarakilishi, Makala za ripoti katika Kiswahili na usemi asili na usemi wa katika Kiswahili.</td></tr>
</table>

## 5.3. Kidato cha tano

### 5.3.1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha tano

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha tano ataweza:

-Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali,

-Kufanya utungaji na ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kwa ufasaha,

-Kufanya ufafanuzi wa kina wa kila utanzu uliopo katika fasihi ya Kiswahili,

-Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi,

-Kuainisha na kubainisha tanzu za fasihi ya Kiswahili na kueleza dhima ya fasihi katika jamii,

-Kufanya mawasiliano rasmi kwa ufasaha akizingatia malengo na nyenzo za mawasiliano zinazotumika,

-Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii kimasimulizi na kimaandishi.

### 5.3.2. Mada za kidato cha tano

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA KUU** | | | **MADA NDOGO** | |
| **I. UWANJA WA FASIHI KAMA SANAA** | | **NADHARIA YA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI** | | **IDADI YA VIPINDI: 72** |
| **Uwezo mahsusi wa mada:** Kufafanua tanzu za Fasihi Simulizi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake; Kubainisha sentensi kulingana na aina zake. | | | | |
| **Malengo ya ujifunzaji** | | | **Yaliyomo** | **Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji** |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | | |
| ➢ Kuonesha tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake.<br>➢ Kueleza dhana ya hadithi simulizi<br>➢ Kueleza dhana ya methali za Kiswahili<br>➢ Kueleza dhana ya nahau na misemo katika Kiswahili<br>➢ Kutaja vitendawili mbalimbali vya kiswahili.<br>➢ Kueleza dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili katika fasihi simulizi na taratibu za | • Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.<br>• Kutunga hadithi simulizi.<br>• Kutumia methali za Kiswahili na kuzihusisha na maisha ya kila siku katika jamii.<br>• Kutumia nahau na misemo ya Kiswahili katika vifungu vya habari mbalimbali<br>• Kutega na kutegua vitendawili mbalimbali katika Kiswahili.<br>• Kughani na kutunga mashairi. | ○ Kuheshimu maonyo kutoka tanzu za fasihi simulizi katika kuimarisha ustawi wa jamii.<br>○ Kuthamini kazi ya utungaji wa hadithi simulizi kama njia ya kurekebisha mwenendo.<br>○ Kujenga busara inayopatikana katika methali.<br>○ Kuimarisha thamani ya lugha kwa kutumia nahau na misemo<br>○ Kukuza fikra na kutatua tatizo haraka.<br>○ Kuendeleza kipaji cha utungaji wa mashairi.<br>○ Kujenga tabia ya kufanya mambo kwa mpango au mwelekeo | ▪ Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake<br>▪ Dhana ya hadithi simulizi<br>▪ Dhana ya methali za Kiswahili<br>▪ Dhana ya nahau na misemo ya Kiswahili.<br>▪ Dhana ya vitendawili vya Kiswahili<br>▪ Dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili | - Katika jozi, wanafunzi watofautishe tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge hadithi simulizi na kuisimulia darasani.<br>- Katika kundi, wanafunzi:<br>a) wachague methali tofauti na kufafanua matumizi yake<br>b) watumie methali mbalimbali katika kifungu cha habari<br>c) walinganishe methali za Kiswahili na Kinyarwanda.<br>- Katika makundi, wanafunzi<br>a) wajadili dhana ya nahau na misemo; b) watoe maana ya nahau na misemo mbalimbali;<br>(c) watunge vifungu vya habari kwa kutumia nahau na misemo tofauti.<br>- Katika jozi, wanafunzi: |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| utungaji<br><br>➢ Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili | • Kutunga na kuchambua sentensi mbalimbali kwa kuzingatia aina zake. | unaopendekezwa. | ▪ Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili (k.m. sentensi sahili, sentensi ambatano, sentensi changamano, n.k.) | (a) wahusishwe katika mchezo wa kutega na kutegua vitendawili tofauti; (b) kueleza muktadha wa vitendawili mbalimbali.<br>- Katika jozi, wanafunzi waghani darasani mashairi mbalimbali; watunge mashairi kwa kuzingatia kanuni za utungaji wa mashairi.<br><br>- Katika jozi, watunge sentensi mbalimbali na kuzichambua kwa kuzingatia aina zake. |
| ***Uhusiano wake na masomo mengine****: Somo la Kinyarwanda , Kiingereza na Kifaransa.* | | | | |
| ***Vigezo vya tathmini au upimaji:*** Kufafanua kwa ufasaha tanzu za Fasihi Simulizi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake; Kubainisha sentensi kulingana na aina zake. | | | | |
| ***Zana/vifaa****: Vitabu vya fasihi simulizi, kazi za fasihi simulizi zilizorekodiwa, michoro, matini na majarida kuhusu fasihi, mtandao wa intaneti, vitabu vya sarufi, tarakilishi.* | | | | |

<table>
<tr><th colspan="3">MADA KUU</th><th colspan="2">MADA NDOGO</th></tr>
<tr><th colspan="3">II. UHAKIKI NA UWASILISHAJI KATIKA FASIHI SIMULIZI</th><th>UHAKIKI WA FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI</th><th>IDADI YA VIPINDI: 72</th></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kuhakiki fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili; Kuchambua sentensi kufuatana na muundo wake.</td></tr>
<tr><th colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</th><th rowspan="2">Yaliyomo</th><th rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</th></tr>
<tr><th>Maarifa na ufahamu</th><th>Stadi</th><th>Maadili na mwenendo mwema</th></tr>
<tr><td>➢ Kueleza dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili</td><td>• Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili pamoja na mbinu za uhakiki.</td><td>○ Kuimarisha tabia ya kusoma na kufanya uhakiki wa kazi zilizosomwa</td><td>▪ Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili</td><td>- Katika kundi, wanafunzi wajadiliane kuhusu a) dhana ya uhakiki wa fasihi simulizi katika Kiswahili; b) umuhimu wa uhakiki; c) mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi simulizi.</td></tr>
<tr><td>➢ Kubainisha vipengele vya uhakiki wa hadithi simulizi</td><td>• Kuchambua hadithi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui.</td><td>○ Kukuza fikra na tafakuri tunduizi katika uhakiki wa kazi za fasihi.</td><td>▪ Uhakiki wa hadithi katika Kiswahili</td><td>- Katika jozi, wanafunzi: (a) wachambue hadithi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui; (b) wafanye tathmini ya hadithi iliyohakikiwa na wengine.</td></tr>
<tr><td>➢ Kueleza matumizi ya methali mbalimbali</td><td>• Kuchambua methali mbalimbali kulingana na vipengele vya uchambuzi.</td><td>○ Kujenga busara, maadili na adabu kupitia methali za Kiswahili.</td><td>▪ Uhakiki wa methali katika Kiswahili</td><td>- Katika kundi, wanafunzi wachambue methali tofauti.</td></tr>
<tr><td>➢ Kubainisha sehemu kuu za kitendawili.</td><td>• Kuchambua vitendawili mbalimbali.</td><td>○ Kufurahia mchezo wa chemshabongo kutokana na kutega na kutegua vitendawili.</td><td>▪ Uhakiki wa vitendawili katika Kiswahili</td><td>- Katika jozi, wanafunzi wahusishe vitendawili mbalimbali na muktadha wake wa asili. K.m. asili ya “Mzungu ametupwa jalalani”</td></tr>
<tr><td>➢ Kueleza muundo wa nahau na misemo katika Kiswahili</td><td>• Kuchambua nahau na misemo.</td><td>○ Kuimarisha tabia ya kuwa wazi na kutumia lugha ya</td><td>▪ Uhakiki wa nahau na misemo katika Kiswahili</td><td>- Katika kundi, wanafunzi wachambue kitendawili kulingana na muundo wake.</td></tr>
</table>

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ➢ Kutambua umbo la shairi simulizi katika Kiswahili.<br><br>➢ Kubainisha sehemu kuu za sentensi | • Kuhakiki shairi<br><br>• Kuchambua sentensi kwa kuonyesha sehemu zake kuu. | mkato katika mawasiliano.<br>○ Kukuza fikra na tafakuri tunduizi katika uhakiki wa mashairi.<br><br>○ Kuwa na utaratibu wa kuainisha, kulinganisha au kutofautisha mambo. | ▪ Uhakiki wa mashairi simulizi katika Kiswahili<br><br>▪ Sarufi: Muundo wa sentensi za Kiswahili: Kiima, kiarifa, shamirisho | - Katika jozi, wanafunzi wafanye uhakiki wa shairi lililotolewa na mwalimu.<br><br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi: (a) achambue sentensi kwa kuonesha muundo wake; (b) atunge sentensi kwa kuonesha kiima, kiarifa, shamirisho na chagizo |
| ***Uhusiano wake na masomo mengine****: Somo la Kinyarwanda, Kingereza, na Kifaransa* | | | | |
| ***Vigezo vya tathmini au upimaji:*** *Kuhakiki fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili; Kuchambua sentensi kufuatana na muundo wake.* . | | | | |
| ***Zana/vifaa****: Vitabu vya fasihi simulizi, kazi za fasihi zilizohakikiwa, michoro ya uhakiki, matini na majarida kuhusu uhakiki, mtandao wa intaneti, tarakilishi.* | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA KUU** | | **MADA NDOGO** | | |
| **III.MAWASILIANO RASMI** | | **UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO** | | **IDADI YA VIPINDI: 38** |
| **Uwezo mahsusi wa mada:** Kuandika barua rasmi, simu na matangazo; Kuchanganua sentensi katika Kiswahili. | | | | |
| **Malengo ya ujifunzaji** | | | **Yaliyomo** | **Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji** |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | | |
| ➢ Kueleza dhana ya barua rasmi na lengo lake<br>➢ Kubainisha sehemu kuu za barua rasmi<br>➢ Kueleza dhana ya simu na mwongozo wa uandishi wake<br>➢ Kueleza dhana ya tangazo na uandishi wake.<br>➢ Kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili. | • Kujadili dhana ya barua rasmi na lengo lake<br>• Kutunga barua rasmi kwa kuzingatia sehemu muhimu zake<br>• Kujadili dhana ya simu kutunga mfano wa simu.<br>• Kuandika matangazo mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo.<br>• Kuandika tangazo kwa usahihi<br>• Kuchanganua sentensi kupitia njia ya matawi, njia ya mishale na njia ya jedwali. | ○ Kuheshimu kanuni za utungaji.<br>○ Kuonyesha ari ya kuboresha mawasiliano kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.<br>○ Kufurahia mawasiliano na wengine kwa matumizi ya vifaa vya kiteknolojia<br>○ Kuimarisha tabia ya kuwasiliana kwa njia ya maandishi sahihi.<br>○ Kufurahia matumizi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili. | ▪ Dhana ya barua rasmi<br>▪ Sehemu kuu za barua rasmi<br>▪ Dhana ya simu na uandishi wake<br>▪ Dhana ya tangazo na uandishi wake<br>▪ Uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili: Njia ya matawi -Njia ya mishale -Njia ya jedwali. | - Katika jozi, wanafunzi wajadili lengo na umuhimu wa barua rasmi.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi: (a) achore kielelezo cha barua rasmi; (b) atunge barua rasmi; (c) afanye tathmini ya barua iliyo na makosa na kutoa mapendekezo yake; (d) ajibu barua iliyoandikwa.<br>- Katika kundi, wanafunzi: (a) wazungumzie dhana ya simu; (b) watunge simu.<br>- Katika kundi, wanafunzi: (a) wazungumzie dhana ya tangazo; (b) watunge tangazo.<br>- Wanafunzi wachanganue tungo mbalimbali kwa kutumia njia ya uchanganuzi iliyotolewa. |
| ***Uhusiano wake na masomo mengine:*** *Somo la Kifaransa, Kiingereza, na Kinyarwanda* | | | | |
| ***Vigezo vya tathmini au upimaji:****. Kutunga barua, simu na matangazo kulingana na mazingira husika na kuchanganua sentensi katika Kiswahili.* | | | | |
| ***Zana/vifaa****: Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa barua, magazeti, mtandao wa internet, vitabu, simu ya mkononi.* | | | | |

<table>
<tr><td colspan="2">MADA KUU</td><td colspan="3">MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="2">IV. KUSOMA NA KUFASILI</td><td colspan="2">UFAHAMU NA UFUPISHO</td><td>IDADI YA VIPINDI: 34</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kufahamu na kufupisha vifungu vya habari mbalimbali; Kutumia kwa usahihi nyakati tofauti za vitenzi.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</td><td rowspan="2">Yaliyomo</td><td rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</td></tr>
<tr><td>Maarifa na ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td></tr>
<tr>
<td>➢ Kueleza dhana ya ufahamu wa habari.<br>➢ Kubainisha taratibu za ufahamu wa kifungu cha habari.<br>➢ Kueleza dhana ya ufupisho wa kifungu cha habari.<br>➢ Kutambua mbinu za ufupisho wa kifungu cha habari.<br>➢ Kubainisha viambishi vya wakati (hali yakinishi na hali kanushi) katika Kiswahili</td>
<td>• Kujadili dhana ya ufahamu wa habari.<br>• Kusoma na kujibu maswali ya ufahamu kutoka kifungu cha habari.<br>• Kufafanua dhana ya ufupisho wa habari na mbinu zake.<br>• Kufupisha kifungu cha habari kwa kuzingatia taratibu za ufupisho.<br>• Kutumia nyakati tofauti kwa usahihi.</td>
<td>○ Kuimarisha tabia ya kusoma vifungu vya habari tofauti.<br>○ Kuwa na utaratibu wa kusoma kifungu cha habari ili kukielewa waziwazi.<br>○ Kuimarisha tabia ya kutumia lugha ya mkato, kuzungumza au kuandika kwa ufupi.<br>○ Kuepuka tabia ya kunakili sentensi au aya wakati wa ufupisho.<br>○ Kujivunia matumizi sahihi ya nyakati katika Kiswahili.</td>
<td>▪ Dhana ya Ufahamu wa habari na taratibu zake<br>▪ Dhana ya ufupisho wa habari na mbinu zake<br>▪ Sarufi: Jedwali la muhtasari wa matumizi ya nyakati katika Kiswahili.</td>
<td>- Katika jozi, wanafunzi wazungumzie dhana ya ufahamu wa habari kwa kusisitizia taratibu zake.<br>- Katika kundi, wanafunzi wasome kifungu cha habari (k.m. usafi wa mwili) na kujibu maswali ya ufahamu (hasa maswali wazi).<br>- Katika jozi, wanafunzi wajadiliane kuhusu dhana ya ufupisho wa kifungu cha habari kwa kuweka mkazo kwenye taratibu zake.<br>- Katika makundi, wanafunzi wasome kifungu cha habari, wakifupishe kisha wawasilishe kazi zao darasani.<br>- Katika makundi, wanafunzi wachore jedwali na kujaza safu kwa kuonesha wakati (k.m. uliopo, uliopita, ujao, wa mazoea, n.k.) na viambishi wakati vyake katika hali yakinishi na hali kanushi.</td>
</tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wake na masomo mengine: Somo la Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kufahamu na kufupisha vifungu vya habari mbalimbali; Kutumia kwa usahihi nyakati tofauti za vitenzi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/vifaa: Vitabu na matini kuhusu ufahamu na ufupisho, mitandao ya intaneti, tarakilishi, vinasasauti, vifungu vya habari.</td></tr>
</table>

## 5.4. Kidato cha sita

### 5.4. 1. Malengo ya somo mwishoni mwa kidato cha sita

Inatazamiwa kwamba mwanafunzi amalizapo kidato cha sita ataweza:

-Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali,

-Kufanya utungaji na ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kama vile hotuba,

-Kufanya ufafanuzi wa kina wa vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa fasihi,

-Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi andishi,

-Kushiriki kwa ufasaha katika midahalo inayohusu mada mbalimbali akitumia Kiswahili sanifu,

-Kufanya ufupisho wa matini za kifasihi na zisizo za kifasihi,

-Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya Jamii kimasimulizi na kimaandishi.

### 5.4.2. Mada za kidato cha sita

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA KUU** | | | **MADA NDOGO** | |
| **FASIHI KATIKA KISWAHILI** | | | **UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI** | **IDADI YA VIPINDI: 72** |
| **Uwezo mahsusi wa mada**: Kutumia tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani; Kutunga sentensi kwa usahihi kufuatana na vifungu vyake. | | | | |
| **Malengo ya ujifunzaji** | | | **Yaliyomo** | **Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji** |
| **Maarifa na ufahamu** | **Stadi** | **Maadili na mwenendo mwema** | | |
| ➢ Kubainisha tanzu za fasihi andishi.<br>➢ Kutambua maana ya hadithi fupi na sifa zake<br>➢ Kufafanua maana ya riwaya na sifa zake<br>➢ Kueleza maana ya tamthilia na sifa zake<br>➢ Kueleza dhana ya ushairi andishi<br>➢ Kuainisha vifungu vya sentensi katika Kiswahili | • Kutofautisha tanzu za fasihi andishi.<br>• Kutunga hadithi fupi kwa kuzingatia muundo wake.<br>• Kutunga riwaya kulingana na muundo wake.<br>• Kubuni au kutunga tamthilia kufuatana na muundo wake.<br>• Kutunga shairi kwa kuheshimu kanuni husika<br>• Kutunga sentensi sahihi kwa mwelekeo wa kirai | ○ Kuimarisha nia ya kusoma tanzu tofauti za fasihi andishi kwa ajili ya mafunzo ya sanaa.<br>○ Kujenga moyo wenye huruma, utu na busara kutokana na maudhui yanayozingatiwa katika hadithi fupi.<br>○ Kukuza stadi za ubunifu katika uandishi wa riwaya.<br>○ Kusisimua watu na kuiburudisha jamii.<br>○ Kukuza kipaji cha utungaji wa mashairi.<br>○ Kuimarisha maarifa ya kuichambua | ▪ Dhana ya tanzu za Fasihi Andishi<br>▪ Utanzu wa hadithi fupi<br>▪ Utanzu wa riwaya<br>▪ Utanzu wa tamthilia<br>▪ Utanzu wa ushairi<br>▪ Sarufi: Virai na vishazi katika Kiswahili | - Katika makundi, wanafunzi waainishe tanzu za fasihi andishi na kuonesha tofauti iliyopo kati yake.<br>- (a) Katika makundi, wanafunzi wajadili sifa za hadithi fupi<br>(b)Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge hadithi fupi kwa kuzingatia sifa zake.<br>- (a) Katika makundi, wanafunzi wazungumzie sifa za riwaya<br>(b) Katika jozi, wanafunzi wasome riwaya moja na kuizungumzia darasani.<br>(c) Kwa kazi ya pekee, mwanafunzi atunge riwaya kulingana na idadi ya kurasa iliyoagizwa na mwalimu.<br>- Katika jozi, wanafunzi (a) wazungumzie sifa za tamthilia; (b) watetee athari za tamthilia, mfano wa Urunana na Indamutsa, katika kuimarisha ustawi wa jamii ya Wanyarwanda; (c) watunge tamthilia yenye urefu uliopendekezwa na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | na kishazi. | sentensi ya Kiswahili kulingana na vifungu vyake. | | mwalimu;<br>(d) Waigize tamthilia darasani.<br><br>- Katika jozi, wanafunzi:<br>(a) wazungumzie dhana ya mashairi andishi;<br>(b) (b) watunge shairi moja kwa kuzingatia sifa zake;<br>(c) waghani shairi fulani.<br><br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi achambue sentensi mbalimbali kwa kuonesha virai na vishazi.<br>- Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kuzingatia vifungu vyake (virai na vishazi.) |

***Uhusiano wa mada na masomo mengine:*** *Somo la Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa.*

***Vigezo vya tathmini au upimaji:*** *Kutofautisha tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili na kufafanua mchango wake katika jamii; kutunga sentensi kwa usahihi kufuatana na vifungu vyake.*

***Zana/Vifaa:*** *Vitabu, majalida, rikoda, vinasa sauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti,tarakilishi*

<table>
<tr><th colspan="3">MADA KUU</th><th colspan="2">MADA NDOGO</th></tr>
<tr><th colspan="3">FASIHI KATIKA KISWAHILI</th><th>UHAKIKI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI</th><th>IDADI YA VIPINDI: 72</th></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kuhakiki kitaaluma kazi mbalimbali za fasihi andishi na kunyambua vitenzi vya Kiswahili.</td></tr>
<tr><th colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</th><th rowspan="2">Yaliyomo</th><th rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</th></tr>
<tr><th>Maarifa na ufahamu</th><th>Stadi</th><th>Maadili na mwenendo mwema</th></tr>
<tr>
<td>➢ Kueleza dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi<br>➢ Kufafanua vipengele vya uhakiki wa hadithi fupi<br>➢ Kueleza vipengele vya uhakiki wa riwaya<br>➢ Kueleza vipengele vya uhakiki wa tamthilia<br>➢ Kubainisha vipengele vya uhakiki wa mashairi<br>➢ Kutambua viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi katika Kiswahili</td>
<td>• Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi pamoja na mbinu za uhakiki.<br>• Kuhakiki hadithi fupi kwa kuzingatia vipengele vyake.<br>• Kuhakiki riwaya kwa kuzingatia vipengele vyake.<br>• Kuhakiki tamthilia kwa kuzingatia vipengele vyake.<br>• Kuhakiki mashairi kwa kuzingatia vipengele vyake.<br>• Kunyambua vitenzi kwa kuzingatia kanuni za mnyambuliko</td>
<td>○ Kuimarisha nia ya kusoma tanzu tofauti za fasihi andishi zilizohakikiwa.<br>○ Kukuza fikra na tafakuri tunduizi.<br>○ Kuendeleza tabia ya utafiti na uhakiki kuhusu kazi za kifasihi<br>○ Kujenga nia ya kushughulikia michezo ya kuigiza na kuihakiki.<br>○ Kuonesha heshima kwa kazi za fasihi andishi na wasanii wake.<br>○ Kujenga maarifa katika kunyambua vitenzi.</td>
<td>▪ Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi<br>▪ Uhakiki wa hadithi fupi<br>▪ Uhakiki wa riwaya<br>▪ Uhakiki wa tamthilia<br>▪ Uhakiki wa mashairi<br>▪ Sarufi: Mnyambuliko wa vitenzi</td>
<td>- Katika makundi, wanafunzi wazungumzie dhana ya uhakiki wa tanzu za fasihi andishi na mbinu za uhakiki.<br>- (a) Katika jozi, wanafunzi wajadili vipengele vya uhakiki wa hadithi fupi<br>(b)Katika makundi, wanafunzi wafanye uhakiki wa hadithi fupi mbalimbali.<br>- Katika makundi, wanafunzi:<br>(a) wazungumzie vipengele vya uhakiki wa riwaya<br>(b) wafanye uhakiki wa riwaya mbalimbali.<br>- Katika makundi, wanafunzi:<br>(a) wazungumzie vipengele vya uhakiki wa tamthilia<br>(b) wafanye uhakiki wa tamthilia mbalimbali.<br>- Katika jozi, wanafunzi:<br>(a) wazungumzie vipengele vya uhakiki wa shairi;<br>(b) wafanye uhakiki wa mashairi mbalimbali.<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi anyambue vitenzi tofauti na kutoa maelezo kwa mnyambuliko wake.</td>
</tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kuhakiki kwa ukamilifu kazi mbalimbali za fasihi andishi na kunyambua vitenzi vya Kiswahili.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Vitabu vya uhakiki wa kazi za fasihi andishi, vinasasauti, simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti, tarakilishi.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th colspan="2">MADA KUU</th><th colspan="3">MADA NDOGO</th></tr>
<tr><th colspan="2">UBUNAJI</th><th colspan="2">HOTUBA NA UFUPISHO</th><th>IDADI YA VIPINDI: 26</th></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kutunga hotuba na kufupisha hati mbalimbali za Kiswahili na kuchambua vitenzi vya Kiswahili kwa njia ya uambishaji.</td></tr>
<tr><th colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</th><th rowspan="2">Yaliyomo</th><th rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</th></tr>
<tr><th>Maarifa na ufahamu</th><th>Stadi</th><th>Maadili na mwenendo mwema</th></tr>
<tr>
<td>➢ Kueleza dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake.<br>➢ Kubainisha taratibu za uchambuzi wa hotuba<br><br>➢ Kueleza dhana ya ufupisho na sifa zake.<br><br>➢ Kutambua mbinu za ufupisho wa habari.<br><br>➢ Kubainisha viambishi vya uambishaji wa vitenzi katika Kiswahili</td>
<td>• Kufafanua dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake.<br>• Kutunga hotuba kwa kuzingatia mwongozo wa utungaji wake.<br>• Kuchambua hotuba kwa kuzingatia taratibu muhimu za uchambuzi.<br>• Kujadili dhana ya ufupisho na sifa zake<br>• Kufupisha habari kwa kuzingatia mbinu za ufupisho.<br>• Kuambisha vitenzi kwa kuzingatia kanuni za uambishaji.</td>
<td>○ Kuimarisha tabia ya kuwa wazi katika hotuba na kutumia msamiati unaofaa.<br>○ Kuheshimu mawazo makuu ya mtu aliyehutubu bila kuyapotosha.<br>○ Kujenga nia ya kulinganisha habari tofauti na ufupisho wake.<br><br>○ Kutilia maanani mbinu za ufupisho ili kuepuka tabia ya kunakili sentensi.<br><br>○ Kukuza maarifa kwa kujishughulisha na mazoezi ya uambishaji wa vitenzi katika Kiswahili.</td>
<td>▪ Dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake<br><br>▪ Uchambuzi wa hotuba<br>▪ Dhana ya ufupisho na sifa zake<br>▪ Mbinu za ufupisho<br>▪ Sarufi: Uambishaji wa vitenzi</td>
<td>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi azungumzie hotuba aliyoisikia au aliyosoma.<br>- Katika jozi, wanafunzi wajadili mwongozo wa utungaji wa hotuba kisha kila mwanafunzi atunge hotuba kuhusu mada mbalimbali.<br><br>- Katika jozi, wanafunzi:<br>(a) wajadili mbinu za uchambuzi wa hotuba;<br>(b) wachambue hotuba mbalimbali kwa kuzingatia sehemu kuu na dhamira iliyomo.<br>- Katika makundi,<br>(a) wanafunzi wajadili dhana ya ufupisho na sifa zake.<br>-Katika makundi, wanafunzi (a) wazungumzie mbinu za ufupisho.<br>(b) Wafanye ufupisho kwa kuzingatia mbinu zake<br>- Katika jozi, wanafunzi washughulikie uambishaji wa vitenzi na kueleza viambishi vilivyohusika.</td>
</tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kutunga hotuba na kufupisha hati mbalimbali za Kiswahili na kuambisha vitenzi vya Kiswahili.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Vitabu kuhusu insha na ufupisho, Kamusi ya Kiswahili sanifu, tarakilishi, hotuba zilizorekodiwa, sarufi kuhusu uambishaji katika Kiswahili.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td colspan="4">MADA KUU</td><td>MADA NDOGO</td></tr>
<tr><td colspan="3">UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO</td><td>MDAHALO NA MJADALA</td><td>IDADI YA VIPINDI: 46</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uwezo mahsusi wa mada: Kuandaa na kuzungumza kwa ufasaha kwenye midahalo na mijadala kwa kuzingatia mada zilizotolewa; Kuambisha vitenzi vya Kiswahili.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Malengo ya ujifunzaji</td><td rowspan="2">Yaliyomo</td><td rowspan="2">Kazi za Ufundishaji na Ujifunzaji</td></tr>
<tr><td>Maarifa na ufahamu</td><td>Stadi</td><td>Maadili na mwenendo mwema</td></tr>
<tr><td>➢ Kueleza dhana ya mdahalo na umuhimu wake katika ujifunzaji wa lugha.<br>➢ Kubainisha taratibu za uandaaji wa mdahalo<br>➢ Kueleza dhana ya mjadala na umuhimu wake katika ujifunzaji wa lugha<br>➢ Kubainisha taratibu za kuandaa na mjadala<br>➢ Kubainisha viambishi vya uambishaji wa nomino na vivumishi katika Kiswahili</td><td>• Kujadili dhana ya mdahalo na mwongozo wake<br>• Kuandaa mdahalo kwa kuzingatia taratibu zake.<br>• Kujadili dhana ya mjadala na mwongozo wake<br>• Kuandaa mjadala kwa kuzingatia taratibu zake.<br>• Kuambisha nomino na vivumishi kwa kuzingatia kanuni za uambishaji.</td><td>○ Kukuza tabia ya kujadiliana na wengine.<br>○ Kuonesha moyo wa heshima, ushirikiano na uwajibikaji wakati wa mdahalo na mjadala.<br>○ Kuendeleza maarifa ya ubunaji wa msamiati wa lugha.</td><td>▪ Dhana ya mdahalo na mwongozo wake.<br>▪ Dhana ya mjadala na mwongozo wake<br>▪ Sarufi: Uambishaji wa nomino na vivumishi</td><td>- Katika jozi, wanafunzi wazungumzie dhana ya mdahalo na mwongozo unaozingatiwa katika uandaaji wake.<br>- Katika makundi, wanafunzi wajadili dhana ya mjadala na mwongozo unaozingatiwa katika uandaaji wake.<br>- Katika makundi wanafunzi waandae na washiriki kwenye midahalo na mijadala kulingana na mada mbalimbali k.v. athari za mavazi ya kisasa, umuhimu wa uzalendo, matumizi ya dawa za kulevya, Ukimwi,n.k)<br>- Kwa kazi binafsi, mwanafunzi ashughulikie uambishaji wa nomino na vivumishi na kueleza viambishi vilivyohusika.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano wa mada na masomo mengine: Somo la hotuba na mjadala katika Kifaransa, Kiingereza na Kinyarwanda.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Vigezo vya tathmini au upimaji: Kushiriki kwa ukamilifu kwenye midahalo na mijadala na kuzungumza kwa ufasaha wakati wa kutoa hoja kwa kuzingatia maagizo husika; Kuambisha nomino na vivumishi kwa kuzingatia kanuni za uambishaji.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Zana/Vifaa: Redio rekoda, vinasasauti, tarakilishi. flash disk, midahalo na mijadala iliyorekodiwa, projekta, n.k.</td></tr>
</table>

## 6. MAREJEO

F.E.M.K, Senkoro (2011). *Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. Kitabu cha kwanza, Kampuni ya Utamaduni, Tafsiri na Uchapishaji (KAUTTU).

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili.* Oxford University Press.

TUKI (1983/2003). *Makala za Semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili I*. Dar es salaam.

NIYOMUGABO, C. (2013). *Mafunzo ya Kiswahili*, *kitabu cha Mwanafunzi (Kidato cha 6*). Fountain Publishers Rwanda Ltd.

Wizara ya Elimu (2010). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kidato cha 4-6*. Taasisi ya Taifa ya Ukuzaji mitaala ( NCDC).

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Shule za Msingi Darasa la I-IV*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2009). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2009). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-VI*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

## 7. VIAMBATISHO

### 7.1. Mgawanyo wa vipindi kwa michepuo husika

| Subject | Weight(%) | Number of periods (Period= 40 minutes) | | |
|---|---|---|---|---|
| **I. Core subjects/Compulsory: Examinable inNational exams** | | **S4** | **S5** | **S6** |
| 1. Literature in English | 14 | 7 | 7 | 7 |
| 2. French | 14 | 7 | 7 | 7 |
| 3. Kinyarwanda | 14 | 7 | 7 | 7 |
| 4. Kiswahili | 12 | 6 | 6 | 6 |
| 5. Entrepreneurship | 6 | 3 | 3 | 3 |
| 6. General Studies and Communication Skills | 6 | 3 | 3 | 3 |
| **Sub-total 1** | | **33** | **33** | **33** |
| **II. Core Subjects: Examinable at School level** | | | | |
| 7. ICT | 6 | 3 | 3 | 3 |
| 8. English | 6 | 3 | 3 | 3 |
| 9. Subsidiary Mathematics | 6 | 3 | 3 | 3 |
| 10. Physical Education and Sports | 4 | 2 | 2 | 2 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Sub-total 2** | | **11** | **11** | **11** |
| **III. Co-curricular activities (compulsory)** | 12 | 6 | 6 | 6 |
| **Total number of contact periods per week** | 100 | **50** | **50** | **50** |
| **Total number of contact hours/week** | | **33.3** | **33.3** | **33.3** |
| **Total number of contact hours per year (39 weeks)** | | **1300** | **1300** | **1300** |